SUMAIT University Journal (SUJ)
ISSN (2507-7864)
Issue No. 11 (December, 2022)

# Umuhimu wa Uwiano kati ya Malengo mahususi na Mazoezi ya Stadi ya Kuzungumza kwa Wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Kigeni

**Salama Said Kahindi**
*The State University of Zanzibar (SUZA), Zanzibar, Tanzania.*
*Kahindis468@gmail.com*

*Received: 1 April 2022, Accepted: 23June 2022, Published: December 2022*
*© SUMAIT University Journal 2022*

**Abstract:**

*When teaching a foreign language, it is important that tasks to improve speaking skills correlate with specific objectives. Various scholars have discussed the concept of correlation in studies about teaching and learning foreign languages. These studies generally confirm that correlation ensures students have an expectation of what is being taught (Kurt, 2020). This study examined the correlation between specific objectives and speaking exercises in a class of learners who are learning Kiswahili as a foreign language. This article explains and emphasizes the importance of correlation in this setting, as the experience showed how some teachers who teach Kiswahili as a foreign language fail to set specific objectives for speaking skill exercises. This article will also show ways of finding out if specific objectives have been achieved, how to correlate specific objectives and exercises, and will demonstrate the importance of correlation between specific objectives and speaking skill exercises. Data for this study was collected through semi structured interviews and documentary analysis. Data was analyzed using a descriptive approach. Research findings have confirmed that teachers were somewhat familiar with the concept of correlation. Therefore, it is recommended that the foreign language teaching center focus on training on correlation in teaching, especially the correlation between specific objectives and exercises that assess students.*

**Keyword: Correlation, specific objectives and speaking exercises**.

**Ikisiri**

Uwiano wa malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza ni muhimu katika ufundishaji wa *lugha ya kigeni. Wataalamu mbalimbali wamejadili dhana ya uwiano katika kusaidia ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za kigeni. Miongoni mwao ni Kurt (2020), ambae aliweza kuthibitisha kwamba uwiano humsaidia kila mwanafunzi kupata matarajio ya kile anachofundishwa. Katika kuliangazia suala hili, makala hii inalenga kufafanua umuhimu wa uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza katika darasa la wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni. Mwandishi wa makala hii ameelezea umuhimu wa uwiano huu kwa sababu uzoefu unaonesha kuna baadhi ya walimu wanaofundisha lugha za kigeni wanashindwa kuoanisha malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza wakati wa ufundishaji. Hivyo, makala hii itaonesha njia za kutambua ikiwa malengo mahususi yamefikiwa, jinsi ya kuoanisha malengo mahsusi na*

*mazoezi ya kuzungumza pamoja na umuhimu wa uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza. Data za utafiti huu zimekusanywa kupitia mbinu za usaili wa nusu funge na uchambuzi wa nyaraka. Data zimechambuliwa kwa kuzingatia mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa walimu wana uelewa juu ya uwiano kwa kiwango cha kuridhisha. Hivyo, imependekezwa kuwa kituo kinachohusika kiongeze juhudi za kuhakikisha kinazidi kutoa mafunzo kwa walimu wake kuhusu uwiano katika ufundishaji wa lugha hasa uwiano wa malengo mahususi na mazoezi kwa ujumla.*

## 1. UTANGULIZI

Stadi ya kuzungumza ni stadi kubwa miongoni mwa stadi kuu nne za lugha zikiwemo stadi ya kuandika, kusikiliza na kusoma (Hussain, 2017). Kuzungumza ni jambo muhimu sana linalozingatiwa na kutiliwa mkazo katika ufundishaji wa lugha, kwa sababu lengo kuu la lugha ni mawasiliano na kuzungumza ni njia moja kuu ya mawasiliano. Katika darasa la lugha ya kigeni, walimu husisitizwa kutumia mkabala wa kimawasiliano ili wanafunzi waweze kuzungumza lugha kwa ufasaha. Makame (2019) anaeleza kuwa, lengo la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni ni kukuza umahiri wa kimawasiliano kwa mjifunzaji badala ya kukuza umahiri wa kiisimu wa lugha hiyo, kwa sababu lengo kuu la lugha ni kuwasiliana. Katika ufundishaji wa lugha ya kigeni, miongoni mwa mambo muhimu ambayo mwalimu huzingatia ni ufahamu wa wanafunzi juu ya mada aliyoisomesha na kuimarika kwa kiwango cha uzungumzaji wa lugha kwa wanafunzi. Kuna njia mbalimbali ambazo mwalimu hutumia kuhakikisha kama wanafunzi wamefahamu, ikiwemo kuwapima kwa kuwapa mazoezi tofauti.

Hata hivyo, mwalimu anapaswa kuzingatia jinsi anavyoipanga mada yake kabla ya kuingia darasani na kuanza kusomesha. Katika upangaji wa mada ni muhimu kuoanisha malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza kwa sababu vitu hivyo vinapowiana huwa ni rahisi kwa mwalimu na wanafunzi kufikia zoezi la ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wamefahamu kila baada ya hatua kwa kuzingatia mrejesho anaoupata kutoka kwa wanafunzi na kutoa msaada pale anapoona unahitajika. Hivyo, mwalimu anayepangilia mada yake kwa kuoanisha malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza, ni vizuri kuhakikisha kuwa anaiwasilisha mada hatua kwa hatua kama alivyopanga na baada ya kuiwasilisha ahakikishe anatathmini ufahamu wa wanafunzi na kuzingatia mrejesho unaopatikana kutoka kwenye majibu ya wanafunzi.

## 2. MAELEZO KUHUSU DHANA MBALIMBALI

### 2.1 Uwiano

Uwiano ni hali ya kulingana kwa fikra au jambo (BAKIZA, 2010:447). Hivyo, makala hii imeangalia uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza yanayotolewa na mwalimu kwa wanaojifuza Kiswahili kama lugha ya kigeni.

### 2.2 Malengo mahususi

Malengo mahususi ni maelezo ambayo mwanafunzi ataweza kuyafanya mwisho wa maelekezo aliyopewa (Mayor, 2016). Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua kuwa, ili mwanafunzi aweze kufanya kwa vitendo maelekezo aliyopewa ni vizuri malengo mahususi yazingatie sifa zake kama vile yaweze kupimika, yaweze kufanyika, yawe na muda maalumu na yawe na uhalisia. Hivyo, mwalimu anapozingatia sifa za malengo mahususi katika uandaaji wa malengo hayo hupelekea mazoezi ya mwanafunzi kuwa rahisi kwa sababu atampima kitu maalum katika ujifunzaji wake.

### 2.3 Mazoezi ya kuzungumza

Mazoezi ya kuzungumza darasani ni kazi anazozitoa mwalimu kwa wanafunzi kwa lengo la kukuza stadi ya kuzungumza. Kazi hizo zinaweza kuwa ni kutunga hadithi, kuzungumza kwa lengo la kupima lafudhi, kusoma kwa sauti na kuelezea vitu mbalimbali (Jyotsna na Rao, 2009). Rubanza (2010:43) anatilia mkazo kuwa lengo kuu la mazoezi ya darasani ni kupima maarifa au kiwango cha stadi wanazotarajiwa wanafunzi kuzijua katika lugha inayohusika. Ni ukweli usiopingika kuwa mtu hujifunza lugha kwa kuzungumza, mtu huweza kuikuza stadi hii pale anapoweza kusikia na kusikiliza sauti, maneno na sentensi mbalimbali kutoka katika mazingira yaliyomzunguka (Anuradha, Raman na Hemamalini, 2014).

## 3. NAMNA YA KUFAHAMU KAMA MALENGO MAHUSUSI YAMEFIKIWA

Mwalimu anapoandaa malengo mahususi anatakiwa ahakikishe kuwa yamefikiwa. Mwalimu anaweza kujua kama malengo yamefikiwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

### 3.1 Ufundishaji wa ana kwa ana

Ufundishaji wa ana kwa ana ni njia ya ufundishaji ambayo huboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kupitia mawasiliano ya kuonana baina ya walimu na wanafunzi (Qureshi, 2019) na (Miles, Mesinga na Zuchowski, 2018). Pia, ni aina ya ujifunzaji maelekezo na vitendo kwa kuhusisha uhamishaji wa taarifa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi (Bandara na Wijekularathna, 2017). Ufundishaji wa ana kwa ana ni njia nzuri na yenye kufaa katika mchakato mzima wa ufundishaji wenye manufaa kwa wanafunzi. Njia hii husaidia sana katika kujua kama malengo ya ujifunzaji yameweza kufanikiwa ama hayakufanikiwa. Ufundishaji huu hujenga na kuongeza maingiliano mazuri baina ya mwalimu na mwanafunzi katika kufundisha na kujifunza, kwani huweza kutoa fursa ya mwalimu na mwanafunzi kuwa wachangiaji wa mada husika. Julien na Dookwah (2020) wanasisitiza kuwa, ufundishaji wa ana kwa ana hupelekea kuongezeka kwa mashirikiano baina ya mwalimu na mwanafunzi. Wanaendelea kuwa, mwanafunzi hujisikia vizuri zaidi na hufahamu kwa urahisi pale anaposoma kwenye mazingira ya darasani anayoyatambua. Vilevile, ufundishaji wa ana kwa ana huwasaidia walimu na wanafunzi kuingiliana na kufahamu jambo linalopelekea kupata taarifa zaidi kuhusu somo husika. Katika ufundishaji wa lugha iwe ya pili au ya kigeni ni vizuri zaidi kujua malengo mahususi yaliyopangwa kwa wajifunzaji ikiwa yameweza

kufikiwa kwa kufanikiwa kutoa mrejesho chanya na hali hii hudhihirisha mafanikio katika ufundishaji.

Wakati wa ufundishaji wa ana kwa ana, wanafunzi wanaweza kujifunza moja kwa moja kwa kumuangalia na kumuiga mwalimu. Hali ambayo, mwalimu huweza kupata mrejesho kwa haraka pale ambapo mwanafunzi amekumbana na ugumu wowote. Pia, katika usomeshaji na ujifunzaji wa ana kwa ana mwalimu anaweza kutambua tatizo la wanafunzi pale tu anapohisi wanafunzi wanauliza maswali sana katika kipengele fulani. Maswali mengi humpa mwalimu ishara ya kutoa msaada wa muongozo kwa kuwafahamisha wanafunzi vizuri sehemu inayowatatiza. Kwa mfano, katika usomeshaji wa stadi ya mazungumzo wanafunzi wanaweza kujifunza kwa mwalimu jinsi ya kutamka maneno mbalimbali, kuzungumza kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa sentensi katika lugha na kuzingatia utamaduni wa lugha husika. Maingiliano yanayotokana na ujifunzaji wa ana kwa ana, si tu yanaruhusu wanafunzi kujipima walichojifunza pia huwaongoza zaidi kukuza tabia ya ushirikiano miongoni mwao. Aidha, ushirikiano wao huwaongezea uwezo wao wa kufahamu, kujiamini na kuacha tabia ya kusoma kwa kujitenga (Chen, 1997).

### 3.2 Kutoa mazoezi ya kumpima mwanafunzi

Upimaji ni kitendo kinachotoa muongozo unaotumiwa kuangalia kama malengo ya ujifunzaji yamefikiwa au la (Sheeba, 2017). Sheeba anaendelea kuwa, kumpima mwanafunzi ni kutambua taaluma ya mtu juu ya kitu ambacho anakijua au amejifunza. Ni ngumu kwa mwalimu kujua kama mwanafunzi amefahamu au hakufahamu kile alichofundishwa mpaka pale atakapoamua kumpima mwanafunzi wake. Kuna njia mbalimbali za kumpima mwanafunzi wa lugha kwa kuzingatia stadi za lugha alizofundisha mwalimu. Hivyo, katika upimaji huo mwalimu hupaswa kuzingatia kiwango cha mwanafunzi na mazoezi anayotoa katika upimaji wake. Mfano katika kiwango cha awali, mwalimu anaweza kumpima mwanafunzi kwa kumuuliza maswali baada ya kusoma matini fulani.

Katika utoaji wa mazoezi ya lugha ya kigeni ni vizuri kwa mwalimu kutoa maelezo rahisi ambayo hayatompa mwanafunzi wakati mgumu wa kuelewa swali. Vilevile, mwalimu anapaswa kutoa muda wa kutosha kwa mwanafunzi ili aweze kufikiri na kujirekebisha mwenyewe. Garbade (2018) anasisitiza kuwa walimu wanaotoa majaribio wawasaidie wanafunzi katika kuwafahamisha maelezo ya jaribio na kuwaruhusu wanafunzi kujisahihisha makosa yao, jambo ambalo huwasaidia wanafunzi kupata ujuzi mpya.

Aidha, upimaji wa mwanafunzi humsaidia mwalimu kujitathmini kwa kujiuliza maswali kama vile alichokisomesha kimefahamika? au je, zana za kufundishia zimesaidia au hazikusaidia kufahamika kwa somo? na zaidi mwalimu ajiulize kama maswali aliyopanga kuwauliza wanafunzi yanaendana na malengo mahususi aliyokusudia kuyafikia. Hivyo, mwalimu anapoweza kujitathmini kwa kujijibu maswali hayo, humsaidia kurekebisha makosa aliyoyafanya na kuwaongoza vizuri wanafunzi kuyafikia malengo aliyokusudia. Ephraim (2016) anasisitiza kuwa kigezo cha kupima mafanikio ya elimu ni malengo. Anaendelea kuwa, matokeo ya upimaji wa mwanafunzi humsaidia mwanafunzi

kujua ameelewa mada kwa kiasi gani, pia humuwezesha mwalimu kugundua malengo ya somo ambayo wanafunzi hawakufanikiwa na kuchunguza sababu. Vilevile, humuwezesha mwalimu kuweza kurekebisha mbinu za kufundishia, kujifunzia na kubuni vifaa vipya ili kuweza kuyafikia malengo mengi zaidi.

### 3.3 Kutoa mrejesho

Mrejesho ni taarifa zinazotolewa kwa wanafunzi kwa ajili kupunguza pengo kati ya uwezo walionao na malengo yaliyopangwa wayafikie (Sadler, 1989). Lengo kuu la mrejesho ni kuwasaidia wanafunzi kupata maarifa zaidi ili kukuza tabia za ujifunzaji wao (Shute, 2008). Mrejesho huweza kutolewa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa wanafunzi, kutoka kwa mwanafunzi kwenda kwa mwanafunzi au kutoka kwa mwanafunzi binafsi yaani, mwanafunzi kuweza kujirekebisha mwenyewe baada ya kukosea (Pearson, 2016). Kila mrejesho anaopewa mwanafunzi ni muhimu sana katika ujifunzaji wake. Kiuhalisia, bila ya mrejesho kutoka kwa mwalimu ni vigumu kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya kigeni kuweza kufahamu vizuri. Mwanafunzi anapomaliza kujibu maswali ni muhimu mwalimu kumuweka wazi kama ameweza au hakuweza. Uwazi huo humsaidia mwanafunzi kujua kosa lake na kujirekebisha wakati huohuo mwalimu huweza kujitathmini. Kwa mfano, mwalimu anaweza kutoa swali au kazi yoyote kama igizo au michezo mbalimbali baada ya kumaliza kusomesha kila hatua muhimu. Mrejesho ni muhimu katika kujua kama malengo yaliyopangwa yamefikiwa ili mwanafunzi aweze kujua makosa aliyoyafanya katika kazi husika. Vilevile, humuongoza mwalimu kutathmini ubora wa mbinu za ufundishaji na humuongoza kufanya mabadiliko yoyote muhimu. Hattie (2011) anasisitiza kuwa, japokuwa mrejesho huonekana kama ni taarifa zinazotolewa kwa ajili ya kurekebisha na kukuza uwezo wa mwanafunzi hata hivyo, mrejesho humsaidia mwalimu kugundua makosa na udhaifu katika njia za ufundishaji alizotumia na kujirekebisha.

### 3.4 Kutumia mbinu shirikishi

Mbinu shirikishi ni aina ya mbinu ya kufundishia ambayo huwahamasisha wanafunzi kushiriki katika uchangiaji wa mada kwa lengo la kupata ujuzi uliokusudiwa (Senthamarai, 2018). Mbinu shirikishi ni miongoni mwa mbinu zinazopendekezwa sana katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Jambo muhimu na la kuzingatia katika utumiaji wa mbinu hii ni kuwaruhusu wanafunzi kujipanga katika vikundi kwa lengo la kujifunza dhana mpya kwa kujadiliana kwa pamoja. Hali hii huongeza kiwango cha ufahamu kwa wanafunzi kutokana na kushiriki katika shughuli zote zinazofanyika darasani wakati wa kujifunza dhana mbalimbali. Mfano wa mbinu shirikishi katika ujifunzaji wa lugha ambazo huweza kutumika ni igizo, maswali na majibu, mjadala, michezo mbalimbali ya kuotea na mengine mengi (Klippel, 1984). Hivyo, mwalimu anahitajika kuwahamasisha wanafunzi kuunda makundi ili washirikiane katika kujifunza mambo mbalimbali. Pia, mwalimu anaweza kushirikiana na wanafunzi na kujua ugumu wa jambo wanalojifunza ili iwe rahisi kuwasaidia kwa kuwaonesha makosa na kuwarekebisha. Aidha, mwalimu atajua kama malengo ya ujifunzaji yamefikiwa au la kutokana na maendeleo ya ushirikiano wa wanafunzi kupitia makundi waliyokaa.

Kwa hivyo, kujua kama malengo mahususi yamefikiwa ni muhimu sana kwani ni katika mafanikio ya mwalimu katika ufundishaji. Kabla ya mwalimu kuanza kusomesha anatakiwa aelewe ni jinsi gani atatathmini malengo yake ili kurahisisha zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji (Disha, h/t).

## 4. JINSI YA KUOANISHA MALENGO MAHUSUSI NA MAZOEZI YA STADI YA KUZUNGUMZA.

Mwalimu anapotaka kusomesha lugha ya kigeni ni vizuri kuhakikisha kwamba mambo matatu ameyachunguza na yamewiana. Mambo hayo ni malengo ya ujifunzaji, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji na kutoa mrejesho (Kurt, 2020).

Katika ufundishaji, mwalimu huandaa malengo ya aina mbili ambayo hutokana na lengo kuu na malengo mahususi. Lengo kuu linahusu ujumla wa mada nzima wakati malengo mahususi yanazingatia kila hatua ya mwanafunzi anayopitia katika mada husika. Hivyo, kwanza mwalimu huandaa lengo kuu la mada halafu huandaa mazoezi kwa kuzingatia malengo mahususi aliyoyaandaa. Mfano katika kitabu cha *Zungumza Kiswahili: Hatua ya Kwanza* (2013) kwenye mada ya *Kujitambulisha*, lengo kuu ni mwanafunzi kujua kujitambulisha na kutambulisha wengine. Malengo mahususi ni mwanafunzi aweze kujitambulisha na kutambulisha wengine ikiwemo majina yao, utaifa wao na kazi zao, mwanafunzi aweze kutumia kitenzi *kuwa* yakinishi na kanushi na pia mwanafunzi aweze kutumia viwakilishi. Kwa kupitia malengo hayo, yamepatikana mazoezi ya kuwataka wanafunzi waigize wakiwa wanajitambulisha na kutambulisha watu wengine. Kuwapa sentensi mbalimbali zenye kitenzi *kuwa* na kubadili kwenda uyakinishi au ukanushi. Vilevile, kutoa mazoezi mbalimbali ya viwakilishi. Uwiano huo kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza hupelekea mwalimu na wanafunzi kufikia malengo kwa urahisi katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji.

Pia, ili kuoanisha malengo mahususi na mazoezi, mwalimu hutumia tathmini kwa ajili ya kuwapima wanafunzi kama wamefikia malengo aliyoyakusudia (Kurt, 2020). Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha kama wanafunzi wamefahamu vizuri mada iliyofundishwa kwa kuwatathmini kwa kuwauliza maswali. Majibu ya wanafunzi yafuatiwe na mrejesho kutoka kwa mwalimu kwa sababu mrejesho husaidia wanafunzi kuelewa makosa yao. Makosa ni jambo lisilo epukika katika kujifunza lugha, makosa humsaidia mwalimu kujua kama wanafunzi wake wameelewa au hawakuelewa kile walichojifunza (Corder, 1987). Hivyo, ili somo lifanikiwe ni vizuri malengo mahususi yawiane na mazoezi ya kuzungumza ili mwalimu aweze kujitathmini na kutathmini vizuri uelewa wa wanafunzi wake.

Ili kuhakikisha mwalimu anajitathmini katika ufundishaji wake, ni muhimu kujiuliza maswali yatakayomsaidia kujua kama mambo yote muhimu katika mada yamewiana. Kurt (2020) ameonesha maswali hayo kama vile, malengo ya ujifunzaji ni yepi? Ni malengo mahususi gani ninayotaka wanafunzi waweze kuyafikia mwisho wa mada hii? Mazoezi gani nitoe? Nitahakikisha vipi wanafunzi wataweza kufahamu mada niliyoikusudia kwa kutumia mazoezi? Nitumie njia gani za

kuwasaidia wanafunzi waweze kufahamu mada kwa urahisi? kazi gani ambazo mwanafunzi ataweza kuzifanya kwa ajili ya kumpima? Kwa hiyo, mwalimu akijiuliza maswali hayo wakati wa kuandaa mada yake, yatamsaidia kupata uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi yoyote atakayoikusudia kuisomesha. Aidha, mwalimu anatakiwa ajitathmini baada ya kusomesha ili kuhakikisha kama amefanikiwa katika ufundishaji wake. Kujitathmini kwake kutahusiana na kuwatathmini wanafunzi wake kwa kuangalia uwezo wao wa kujibu maswali anayowauliza. Endapo hawakufahamu, mwalimu hatakiwi kukata tamaa bali anatakiwa ajitathmini upya kupitia njia alizotumia ili kurekebisha alipokosea.

## 5. UMUHIMU WA UWIANO KATI YA MALENGO MAHUSUSI NA MAZOEZI YA STADI YA KUZUNGUMZA

Kuoanisha malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza wakati wa ufundishaji ni jambo muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha hasa lugha ya kigeni kwa sababu zifuatazo:

### A. Husaidia kukuza ufahamu wa wanafunzi

Malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza yanayotolewa na mwalimu darasani yanapowiana huwa ni rahisi kwa mwalimu kufikisha alichokusudia pia ni rahisi kwa wanafunzi kufahamu haraka walichofundishwa. Ni vizuri kila baada ya hatua, mwalimu atoe mifano pamoja na mazoezi yanayoendana. Mifano ambayo itamuongoza mwanafunzi kufahamu zaidi na kuweza kujibu maswali atakayopewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwaonesha wanafunzi video za maamkizi rasmi na maamkizi yasiyo rasmi. Baada ya kuwaonesha video hizo zaidi ya mara tatu mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi waigize aina za maamkizi waliyojifunza. Pia, katika kitabu cha *Zungumza Kiswahili: Hatua ya Kwanza* (2013:3) kwenye mada ya *Maamkizi*, baada ya mwanafunzi kusoma majibizano ya aina za maamkizi anatakiwa kufanya zoezi la igizo la maamkizi aliyojifunza.

Kwa wanafunzi, mazoezi ya kuzungumza ni muhimu sana kwa sababu mwanafunzi anapoweza kuzungumza maana yake ameweza kufahamu ujumbe aliousikia kwani binaadamu hawezi kuzungumza peke yake. Mazungumzo ni baina ya watu wawili ambao hutoa kauli kila mmoja kwa wakati wake (Timothy, 2016). Kuweka wazi uhusiano wa malengo mahususi na mazoezi husaidia kuhakikisha wanafunzi wanafahamu dhamira iliyolengwa pamoja na kufanikisha ufikiwaji wa mada.

### *B. Humsaidia mwanafunzi kuweza kutumia lugha katika mazingira halisi*

Malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza yanapowiana humrahisishia mwalimu katika kumuandaa mwanafunzi kuweza kuitumia lugha katika mazingira halisi. Baada ya mwalimu kuweka usawa kati ya kufuata mtaala na matakwa ya wanafunzi, kinachofuata ni kuhakikisha uwiano baina ya malengo mahususi aliyoyapanga na mazoezi aliyoyakusudia kuwapima wanafunzi. Uzoefu unaonesha lengo kuu la wanafunzi wanaojifunza lugha nyengine ni kuweza kuwasiliana kwa kutumia

lugha wanayojifunza. Ili wanafunzi wakuze uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia lugha lengwa, wanahitaji wapewe fursa mbalimbali za kuifanyia lugha mazoezi (Brandl, 2007). Mazoezi hayo ni yale ya shughuli za msingi za kazi (Task Based Activities) (Kawasaki, 2021). Kawasaki anaendelea kuwa, shughuli za msingi za kazi ni mazoezi ambayo mwanafunzi anayafanya kwa kutumia lugha lengwa kwa ajili ya kufikia lengo fulani. Shughuli nzuri ni zile zinazoakisi hali halisi ya maisha ili wanafunzi waweze kuona muingiliano baina ya somo na mazingira halisi. Mfano mwanafunzi anaweza kupewa kazi ya kumuelekeza mtu njia, kuagiza chakula mkahawani, kupanga safari na kuongoza kikao. Walimu wanatakiwa watoe mazoezi tofauti yanayoendana na mazingira ili kuwapa wanafunzi fursa mbalimbali za kujifunza lugha kwa kuzungumza (Burk, 2016). Vilevile, mwalimu anapotoa mazoezi ni vizuri kuangalia wanafunzi wameyapokea vipi kutokana na jinsi wanavyojibu maswali na wengine wanavyopokea kama wamefahamu au la. Hivyo, mrejesho ni muhimu sana hata kwa wanafunzi waliofahamu, hii itawasaidia wazidi kujifunza mambo mengi mapya yatakayosaidia kukuza uwezo wao wa kuzungumza katika mazingira halisi. Mwanafunzi kuweza kuzungumza lugha kwa ufasaha kunatokana na utayari wake mwenyewe. Utayari wa mwanafunzi hutokana na hamasa, kujitolea kuwasiliana, kushiriki darasani, kuitafuta na kuitumia fursa ya kuzungumza na kuzishinda changamoto mbalimbali ikiwemo aibu na kukata tamaa (Burk, 2016). Hivyo, kuwiana kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza humsaidia sana mwanafunzi kuielewa vizuri stadi ya kuzungumza na kuweza kuitumia lugha katika mazingira halisi.

***C. Humsaidia mwanafunzi kuielewa vizuri stadi ya kuzungumza***

Stadi ya kuzungumza ni miongoni mwa stadi kuu nne za lugha zikiwemo stadi ya kusoma, kuandika na kusikiliza. Binaadamu huwasiliana kwa kutumia mazungumzo, hivyo, lugha ya mazungumzo ni lugha inayozingatiwa sana kuliko lugha ya maandishi (Ali, 2015). Katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni stadi ya kuzungumza ni stadi inayopewa kipaumbele na walimu kutokana na kufuata mkabala wa kimawasiliano. Walimu hutumia njia mbalimbali pamoja na kutoa mazoezi tofauti ili kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kuzungumza. Hata hivyo, kutokana na matokeo ya utafiti huu, kutumia njia za ufundishaji na kutoa mazoezi mengi bila ya kufanya uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza ni vigumu kwa wanafunzi kuielewa lugha vizuri na kuweza kuzungumza kwa urahisi. Kwa mfano, katika mada ya *Maamkizi,* kumpa mazoezi mwanafunzi anaejifunza lugha ya Kiswahili kusalimia watu bila ya kumuelekeza aina za maamkizi ya Waswahili, mwanafunzi atachukua muda mrefu kujifunza salamu.

Hivyo, malengo mahususi ni vizuri yaendane na mazoezi ya stadi ya kuzungumza kwa sababu mazoezi hulenga kupima ufikiwaji wa malengo mahususi. Kama mwalimu ameandaa malengo mahususi yenye lengo la kukuza uwezo wa kuzungumza na mazoezi yake hayakuzingatia stadi ya kuzungumza basi lengo la mwalimu halitafikiwa. Kwahivyo, ili kumfanya mwanafunzi wa lugha ya kigeni kuelewa vizuri stadi ya kuzungumza na kuweza kuzungumza ni vyema mwalimu kuwa makini katika kuoanisha malengo mahususi na mazoezi mbalimbali yanayolenga kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza.

### *D. Wanafunzi wataweza kupata ujuzi*

Malengo mahususi ni malengo yanayoelezea kitu gani wanafunzi wajue au waweze kukijua mwishoni mwa mada ambacho mwanzo walikuwa hawakijui (Wanjohi, 2014). Katika kila lengo mahususi moja hulenga kupata ujuzi mpya. Hivyo, malengo mahususi na mazoezi yanapowiana huwa ni rahisi sana kwa wanafunzi kuelewa ujuzi huo. Kwa mfano katika mada ya *Mkahawani* kwenye kitabu cha *Zungumza Kiswahili: Hatua ya Kwanza* (2013), malengo mahususi yake ni (a) mwanafunzi aweze kuagiza chakula na kinywaji katika mkahawa, (b) mwanafunzi aweze kufanya malipo, (c) mwanafunzi aweze kutumia wakati uliopo kanushi na yakinishi, (d) mwanafunzi aweze kutumia ngeli ya ki-vi na (e) mwanafunzi aweze kuhesabu 1-1000. Kwa kupitia malengo mahususi hayo, kwa kawaida mwalimu huanza kufundisha na kufuatiwa na mifano, halafu mazoezi kwa lengo moja baada ya jengine ili kuhakikisha kila mwanafunzi anaelewa na kupata ujuzi wa kila lengo.

Mwalimu huweza kujua kama wanafunzi wamefahamu kila lengo kutokana na tathmini atakayoitoa kila baada ya kumaliza kufundisha lengo moja. Tathmini hiyo itazingatia ujuzi walioupata wanafunzi baada ya kusomeshwa na kutolewa mazoezi yaliyoendana na malengo mahususi. Kutokana na mada ya *Mkahawani* na malengo mahususi yake kama yalivyoainiswa hapo juu, itamlazimu mwalimu kutathmini kama wanafunzi wameweza kuagiza chakula na vinywaji, kama wameweza kufanya malipo baada ya kuhudumiwa, kama wameweza kutumia wakati uliopo kanushi na yakinishi wakati wa mazungumzo yao, kama wameweza kutumia ngeli ya ki-vi na pia kama wanafunzi wameweza kuhesabu 1-1000. Kwa hivyo, tathmini ya mwalimu itaweka wazi kama wanafunzi wameweza kupata ujuzi uliokusudiwa au la. Baada ya mwalimu kuridhika na tathmini yake anatakiwa kufanya maamuzi sahihi, kama wanafunzi hawakuweza kupata ujuzi basi ni vizuri mwalimu kutoa mrejesho utakaowasaidia wanafunzi kuyajua na kurekebisha makosa yao ili kufikia hatua ya kupata ujuzi uliokusudiwa.

## 6. MAPENDEKEZO

Elimu zaidi inahitajika kwa walimu juu ya uwiano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi nyengine kama stadi za kusoma, kuandika na kusikiliza. Pia, sambamba na kutoa elimu juu ya umuhimu wa uwiano kati ya malengo mahususi na stadi nyengine. Elimu hizi ni muhimu zaidi katika ufundishaji wa lugha ya kigeni kwani stadi zote ni muhimu sana kwa wanafunzi, hivyo zinapofikiwa kwa undani ni rahisi kwa wanafunzi kuielewa lugha kwa undani zaidi.

Kuweka wazi njia nyengine za kuweza kujua kama malengo mahususi yamefikiwa au la. Hii itazidi kuwasaidia walimu kuhakikisha wanafikisha kwa urahisi walichokusudia kukifundisha.

## 7. HITIMISHO

Ni muhimu kwa walimu kuzingatia mfanano kati ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza. Vilevile, mwalimu ahakikishe anazingatia njia za kujua kama malengo mahususi yamefikiwa na wanafunzi kwa sababu kufikiwa kwa malengo mahususi na wanafunzi ni hatua

muhimu katika zoezi la ufundishaji na ujifunzaji. Kazi hii itawasaidia wadau wote wa lugha wakiwemo walimu wa lugha hasa walimu wa lugha ya kigeni kupata ufahamu juu ya umuhimu wa uwiano baina ya malengo mahususi na mazoezi ya stadi ya kuzungumza yanayotolewa na walimu darasani.

**MAREJEO**

- Ali, L. H. (2015). *Changamoto na mbinu za kiisimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa elimu ya awali*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Anuradha, R. V., Roman, G. & Hemamalini, H.C. (2014). *Methods of teaching English*. Neelkamal Publication.
- BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Oxford University Press.
- Bandara, D. & Wijekularathna, D.K. (2017). Comparison of student performance under two teaching methods: Face to face and online. *The International Journal of Educational Research, vol 12 (1), pg 69-79.*
- Brandl, K. (2007). *Communicative language teaching in action: Putting principles to work*. Upper saddle river.
- Burk, J. J. (2016). *Language learning for real-world context*. (Master's research) Utah state University
- Chen, L. (1997). Distance delivery systems in terms of pedagogical considerations: A revolution. *Educational Technology, vol 37 (4), pg 34-37.*
- Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. (2013). *Zungumza Kiswahili: Hatua ya kwanza.* Educational Books Publishers Ltd.
- Corder, S. (1987). *Error analysis and interlanguages*. Oxford University Press.
- Disha, M. (n/d). *Evaluation in teaching and learning Process*.
- Ephraim, E. (2016). *Upimaji na tathmini*. https://www.sribd.com/ documen t /3299 12066/ upimaji-tathmini-pdf
- Garbade, M. J. (2018). *Four tricks to know if eLearning objectives are met*.
- Hattie, J. (2011). Feedback in schools. In R. Sutton., M. J. Hornsey. & K. M. Douglas (Eds.), *Feedback: The communication of praise, criticism and advice*. Peter Lang Publishing.
- Hussain, S. (2017). Teaching speaking skills in communication classroom. *International Journal of Media, Journalism and Mass Communication, vol 3, issue 3, pg 14-21.*
- Julien, G. & Dookwah, R. (2020). Student's transition from face to face learning to online learning at higher education: A case study in Trinidad and Tobago. *Academic Journals, vol 15 (8), pg 487-494.*
- Jyotsna, M. & Rao, S. N. (2009). *Methods of teaching English*. New Era Publication
- Kawasaki, J. (2021). *What is task based learning? A guide to the popular teaching method*. https://bridge.edu/tefl/blog/what-is-task-based-learning/#
- Klippel, F. (1984). *Keep talking: communicative fluency activities for language teaching*. Cambridge University Press.
- Kurt, S. (2020). *How can we align learning objectives, instructional strategies and assessment?*

- Makame, K. O. (2019). Mkabala wa kimawasiliano katika ufundishaji wa lugha ya pili: Mifano kutoka ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni Tanzania. *African Journals Online, vol 82 No. 1 (2019).*
- Mayor, M. (2016). *SMART objectives for smart teachers*. Pearson
- Miles, D., Mesinga, J. & Zuchowski. (2018). Harnessing opportunities to enhance the distance learning experience of MSW students: An Appreciative Inquiry Process. *Social Work Education, 37 (6), pg 705-717.* https://doi.org/10.1080/02615479.2018.1447557
- Pearson. (2016). *Providing educational feedback*. https://www.pearson. com/content/ dam/one-dot-com/one-dot-com/us/en/pearson-ed/downloads/Feedback.pdf
- Qureshi, J.A. (2019). Advancement in massive open online courses (MOOCs) to revolutionize disruptive technology in education: A case of Pakistan. *Journal of Education and Educational Development, vol 6(2), pg 219-234.*
- Rubanza, Y. I. (2010). Masuala ya msingi katika utayarishaji wa majaribio kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. *Kioo cha Lugha, Juz 8.*
- Sadler, D. R. (1989). Formative assessment and the design of instructional systems. *Instructional Science, vol 18 (2), pg 119-144.*
- Senthamarai, S. (2018). Interactive teaching strategies. *Journal of Applied and Advaned Research, vol3.*
- Shute, V. (2008). Focus on formative feedback. *Review of Educational Research.* Princeton, NJ: Educational Testing Services. https://wwwresearchgate.net /publication/ 220017728_Focus_on_Formative_Feedback
- Sheeba. (2017). Importance of testing and evaluation in teaching and learning. *International Journal of Society and Humanities, vol 11, No 1, pg 1-9.*
- Timothy, K. M. (2016). *Maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii husuani Facebook na Twitter* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wanjohi, J. M. (2014). *Research objectives*. http://sps.uonbi.ac.ke.